

MAFANIKIO YA LATRA SIKU 100 ZA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Sekta ya usafirishaji inamchango mkubwa kwa ukuaji wa uchumi. Ili kuchochea zaidi ukuaji wa uchumi, mwaka 2019, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhi (LATRA) chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhi, Sura ya 413. Lengo kuu lilikuwa ni kudhibiti huduma za usafiri ardhi kupitia barabara, reli, na usafiri wa waya. Tangu kuanzishwa kwake, LATRA imeleta mabadiliko makubwa na kutatua changamoto zilozokuwepo awali, ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za usafiri wa umma.

Mafanikio ya LATRA yamewezeshwa na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Uchukuzi. Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na ubunifu katika udhibiti wa usafiri, hali inayoongoza uwekezaji na kuwezesha mitaji kuwa endelevu. Wizara ya Uchukuzi chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akisaidiwa na Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi na Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, wamefanya jitihada za makusudi kuhakikisha Mamlaka inatekeleza majukumu yake kwa kusimamia vizuri sekta ya usafirishaji nchini na kuhakikisha wadau kupata huduma bora, salama, na endelevu. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 ambapo LATRA ilianzishwa hadi sasa, Mamlaka imepata mafanikio makubwa kupitia utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

KUKUZA MATUMIZI YA TEHAMA KWENYE UTOAJI WA HUDUMA

Serikali imeendelea kuiwezesha Mamlaka kubuni na kutengeneza Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo imekuwa ikitumika katika shughuli mbalimbali za kiudhibiti. LATRA imeonesha mafanikio makubwa katika kudhibiti na kuboresha huduma za usafiri ardhi nchini Tanzania, huku ikichangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Mafanikio haya ni matokeo ya uwajibikaji wa hali ya juu na ushirikiano wa karibu kati ya Mamlaka, Serikali, na wadau wa sekta ya usafirishaji.

Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS)

LATRA inazingatia ubunifu na haswa matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa kazi. Katika kipindi hiki, LATRA imehuisha Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS) mms.latra.go.tz/ ambao ni mfumo mkuu wa utaji leseni, usajili madereva, malipo na taarifa za udhibiti. Mfumo wa RRIMS umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mfumo wa Malipo ya Kielektroniki Serikalini (GePG) na Mamlaka ya Usajili na Leseni za Biashara (BRELA) ili kurahisisha uhakiki. Kadhalika, Mfumo huu unamuwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 bila uhitaji wa kufika ofisi za LATRA, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa usumbufu na muda wa kupata huduma.

Ufanisi wa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

Mfumo wa kufuatilia mwenendo wa magari umeimarisha usalama barabarani, huku ukiunganisha magari 13,574 yaendayo mikoani na nchi jirani. Mfumo huu pia umeboresha uchunguzi wa ajali na kurahisisha usimamizi wa ratiba za madereva. Aidha, LATRA imeongeza idadi ya leseni za usafirishaji zinazotolewa kila mwaka kupitia ofisi za LATRA na mawakala walioidhinishwa.

Jedwali : Idadi ya Leseni Zilizotolewa na LATRA

SN	Aina ya Huduma	2020/21	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25
1	Mabasi (PSV)	49,280	47,547	50,939	48,349	51,264
2	Malori (GSV)	141,633	143,011	169,942	192,996	210,749
3	Pikipiki na Bajaji	38,106	43,728	57,449	68,554	75,820
4	Teksi kawaida	291	2,654	2,305	2,345	2,381
5	Tax Mtandao	943	3,013	3,523	13,402	11,946
6	Magari ya kukodi	-	-	718	930	1,031
	Jumla	230,253	239,953	284,676	326,576	353,191

Chanzo: LATRA

Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) – Safari Tiketi

LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) pamoja na wadau wengine, imesanifu na kutengeneza Mfumo wa Safari Tiketi ambao ni Mfumo Jumuishi wa Ukataji Tiketi unaowezesha abiria kukata Tiketi za Treni na Mabasi Kiganjani unaopatikana kwa anwani tiketi.latra.go.tz au kwa kupakua kwenye simu janja. Mfumo huu umeunganishwa na mifumo mingine ya utaji tiketi ikiwemo wa TRC na mifumo ya tiketi za mabasi ili kurahisisha ukataji tiketi na kutunza taarifa za abiria. Mfumo huu umeondoa ulanguzi wa nauli, umewasaidia abiria kukata tiketi bila kwenda kwenye ofisi ya basi au stesheni na umewezesha abiria kulipa nauli halali zilizo idhinishwa na Serikali, umeimarisha ukusanyaji wa mapato ya wamiliki wa mabasi bila kupitia mtu wa kati, umesaidia wamiliki wa mabasi kupata faida endelevu na kuboresha huduma kwa abiria. Aidha kupitia mfumo huu wasafirishaji wanaaminika zaidi na taasisi za kifedha na kukopesheka kwa urahisi kutokana na mapato yao kuingia katika akaunti zao za benki moja kwa moja.

Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App)

LATRA imehuisha Mfumo Tumizi unaopatikana kwenye simujanja unaomuwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi, kufanya uhakiki wa tiketi, kutambua halali wa leseni za magari na adhabu, hivyo kumuwezesha abiria kuepuka kutumia ghali lenye changamoto ili kujiepusha na usumbufu. Pia Mfumo huu umeunganishwa na Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (PIS) unaomuwezesha abiria kufahamu vituo vya mabasi Tanzania Bara, kufahamu eneo basi lilipo, na kufuatilia mwendo wa basi



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

husika likiwa safarini.

Mfumo wa Huduma kwa Wateja

LATRA imeendelea kutumia Mfumo Jumuishi wa Serikali wa Huduma kwa Wateja kupitia kituo cha huduma kwa wateja kinachofanya kazi kwa saa ishirini na nne (24) ili kurahisisha utatuzi wa migogoro na changamoto kwa wakati. Huduma za kituo hicho zinapatikana kupitia namba za kupiga bila malipo 0800110019 na 0800110020. Vilevile Mamlaka imeendelea kuzitangaza namba hizi kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii na kuzibandika katika maeneo mbalimbali yanayofikiwa na wadau wetu. Aidha, namba hizi zinaandikwa kwenye milango ya mabasi ya mijini sambamba na viwango vya nauli.

Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho

LATRA imeendelea kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali wa e-Mrejesho unaotumika kwa Kutuma, Kupokea na Kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi. Mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa anwani wa emrejesho.gov.go.tz/ au kwa kupakua mfumo tumizi wa e-Mrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) kwa kubofya namba *152*00# au kwa kupitia tovuti ya LATRA www.latra.go.tz sehemu ya tovuti mashuhuri. Hivyo, Mamlaka inawasihia wananchi wote kutumia mfumo huo na masuala yatakayowasilishwa yatashughulikiwa ndani ya siku 21 tangu ya lipowasilishwa.

UTENGENEZAJI WA KANUNI MPYA ZA USAFIRI ARDHINI NA USHIRIKISHWaji WA WADAU

LATRA pia imefanikiwa kushiriki katika utengenezaji wa kanuni mpya za usafiri ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali chini ya uongozi wa Wizara ya Uchukuzi. Ushirikishwaji wa sekta binafsi umekuwa muhimu katika kuhakikisha masuala yanayowahusu wadau yanashughulikiwa na kupatiwa suluhisho kwa pamoja. Miongoni fursa zilizowezeshwa na kanuni mpya za mwaka 2023 na 2024 ni pamoja na kuruhusu mawakala wa kutoa leseni za LATRA ambapo mawakala hao hujipatia kipato kwa kurejeshewa 20% ya mapato yatokanayo na leseni husika. Aidha, maboresho ya kanuni, pamoja na mambo mengine yamepunguza viwango vya tozo za adhabu na utaratibu wa kutoa onyo kabla ya adhabu kwa baadhi ya makosa katika huduma za usafiri.

Hadi sasa fursa hizo zimeanza kuwanufaisha wadau kama vile Chama cha Akiba na Mikopo cha Bajaji na Bodaboda Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS), Kampuni ya Balagumu Investment inayotoa huduma za uwakala za leseni kwa mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga na Rukwa, Ushirika wa usafirishaji mkoa wa Mwanza (UWAMWA) pamoja na Chama cha Kuweka na Kukopa cha Maafisa Usafirishaji wa Pikipiki Dar es Salaam (MAUPIDA SACCOS) wanaendelea na utaji wa leseni za LATRA kwa wanachama wao baada ya kupewa cheti cha LATRA cha ridhaa ya kutoa leseni za usafiri wa pikipiki, usafiri wa taksi na magari maalum ya kukodishwa.

SAFARI ZA MABASI KWA SAA 24

Serikali ilirejesha huduma za mabasi kwa saa 24 kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2023 baada ya kuzingatia maoni ya wadau na hali ya usalama barabarani. LATRA imeendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usafiri kwa safari za usiku kupitia ikifumo na kaguzi zinazoendeshwa na LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani. Mamlaka imeendelea kuhakikisha madereva wanaoendesha safari za usiku ni wale waliothibitishwa na wanaotumia kitufe cha utambuzi wa dereva (i-Button) wakati wote wa safari. Hatua hii imeimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja, wasafirishaji, na Serikali kwa ujumla kwa kuwa huduma hizo zimerahisisha ratiba za abiria kijamii na kibiashara.

HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI

Katika sekta ya reli, LATRA imehakikisha ubora wa miundombinu na mabehewa ya reli ya kisasa (SGR). Semina za usalama kwa wafanyakazi wa reli zimeimarisha uendeshaji wa shughuli za reli, na kuboresha huduma kwa abiria. Kwa upande wa usafiri wa waya, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imeendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wawekezaji. Hadi sasa rasimu ya Kanuni za udhibiti wa usafiri wa waya ziliandaliwa na maoni ya wadau yalitolewa na kuwekwa kwenye Kanuni ambazo zipo katika hatua za mwisho kutangazwa na kuanza kutumika. Usafiri wa waya hutumika katika maeneo mbalimbali ikiwemo yenye milima na vivutio vya utalii kama Arusha na Kilimanjaro. Hii ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii nchini ambapo kwa sasa idadi ya watalii imeongezeka.

06034002

Latra targets 260 new buses to address transport gaps in Dar

By Hellen Nachilongo
@musanachi60
hnachilongo@
tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. The Land Transport Regulatory Authority (Latra) has announced eight new commuter bus routes and identified several existing routes that require additional vehicles, in a move aimed at easing transport challenges in the city.

Latra's head of public relations and communications, Mr Salum Pazy, said three existing routes require an additional 60 buses, while the eight new routes will require 200 buses.

The new routes include: Videte-Buza via Mvuti to Kilungule; Videte-Mbezi Luis via Mvuti; Kuvule-Malamba Mawili; Videte-Kivule Hospital via Mvuti; Msongola-Fremu Kumi; Videte-Tabata Segerea via Nyerere to Majumba Sita; Mburahati Sokoni-Mlonganila via Maji Chumvi, Morogoro; and Mbezi-Tegeta Nyuki via Msumi to Mandale.

Routes earmarked for additional vehicles include

Mwenge Stand-Mnazi Mmoja via TRA, Tandale Sokoni and Kawawa to Uhuru; and Mwanagati-Mnazi Mmoja via Banana to Nyerere, as well as Mwanagati-Muhimbili via Banana to Nyerere.

Mr Pazy said a total of 260 buses, each with a minimum seating capacity of 25 passengers, are required to serve the identified routes.

He stressed that only vehicles with registration numbers beginning with "DAA" will be eligible for licensing, and that all drivers must be officially registered and approved by Latra to operate legally.

The requirements, he said, are intended to ensure orderly and professional service delivery as Dar es Salaam continues to expand and invest in transport infrastructure.

The number of buses that will be assigned to three existing routes among the needed 260

60

The secretary general of the Dar es Salaam Commuter Bus Owners Association (Darcoboa), Mr Shifawaya Lema, welcomed the move, saying the introduction of new routes would create business opportunities for operators and improve service coverage.

"Although I have not yet seen Latra's official statement, the introduction of new routes would allow more operators to deploy their commuter buses. It is also an opportunity for bus owners who have long observed demand along those corridors," he said.

Mr Lema noted that operators are often cautious about investing in newly introduced routes, but passenger uptake typically grows over time.

"For example, when the Mnazi Mmoja-Mbezi via Maji Chumvi route was first introduced, many operators were reluctant because of the high number of three-wheelers operating around Kimara. Today, however, it has become one of the busiest routes, widely used and appreciated by passengers," he said.

ECOSYSTEM The initiative targets small business owners and startups

Zanzibar startups get funding boost

The Zanzibar Business Plan Competition, which opened on January 15 and will run until March 15, 2026

The Citizen Reporter
@TheCitizenTz
news@tz.nationmedia.com

Zanzibar. A new initiative aimed at financing and supporting high-potential entrepreneurs across Zanzibar is taking shape, in what organisers describe as a milestone for the islands' startup and small business ecosystem.

The Zanzibar Business Plan Competition, which opened on January 15 and will run until March 15, 2026, targets small business owners, startups, and early-stage entrepreneurs based in Zanzibar who are seeking both capital and structured support to scale viable business ideas.

It was formally launched by the Coprosperity Fund at Mercury's in Stone Town,



Managing Partner at the Coprosperity Fund, Mr Antony Adolf (left) and the organisation's Marketing and Communications manager, Linda Mkwawa, display the banner of the competition. PHOTO | COURTESY

with a particular focus on | tical business planning tool,